



Press Release 21st May 2011

Contact Information:
Lilian Nsemwa
Public Relations Advisor
Lilian@feminahip.or.tz
0752108723
www.feminahip.or.tz
www.chezasalama.com



Ruka Juu na Fema TV Talk Show

<<Name of winner>> ndiye mshindi wa shindano la ujasiriamali la Ruka Juu na Fema TV talk show. Mjasiriamali huyu amejishindia shilingi za kitanzania milioni tano taslimu (Tshs. 5,000,000) ili kuendeleza biashara yake.

Ruka Juu ilianza kurushwa hewani tarehe 21 mwezi Machi mwaka huu na tumeshuhudia ilivyofanikiwa kuzikonga nyoyo na kuziteka akili za watanzania wengi. Vijana sita wajasiriamali wamekuwa wakishindania fursa hii ya kipekee katika maisha yao.

Watazamaji wamekuwa wakishiriki kwa kutuma ujumbe mfupi wa SMS, kwa kupiga kura pamoja na kutoa maoni yao. *“Ruka Juu, napenda show yenu kwa kuwa inasaidia vijana, akina mama na akina baba kujikomboa kutoka katika hali ngumu ya maisha”.*

Ruka Juu na Fema TV Talk Show ni mpango wa Femina HIP kufuatia tatizo la ajira, vijana zaidi ya milioni moja wanamaliza shule na vyuo kila mwaka tayari kwa kuingia katika soko la ajira. Wanatarajia kupata ajira, lakini fursa za ajira ni chache tu na hivyo vijana wengi inabidi wajijiri na kutafuta njia zao wenyewe za kujipatia kipato.

Ruka Juu ni kipindi cha kwanza cha luninga cha Femina HIP kinachoonyesha uhalisia wa mambo katika nyanja ya ujasiriamali na elimu ya mambo ya fedha. Ni shindano lililoandaliwa ili kuwafanya watazamaji wafikiri, wapange na wachakarike kufanya kazi ili kujenga maisha yao.

Leo hii Femina HIP ni asasi kubwa ya kiraia yenye mkakati wa elimu na upashanaji habari unaofanya kazi na vijana, jamii na washirika kote nchini Tanzania. Tunashirikisha zaidi ya watu milioni kumi kila wiki kupitia **machapisho, luninga, redio, mtandao wa intaneti, SMS na mazungumzo ya uso kwa uso**. Kupitia jukwaa hili la Ruka Juu tumeweza kuelimisha kuhusu namna ya kumjali mteja, kupata stadi za fedha, kuanzisha na kusajili biashara, na namna ya kuchagua mitindo bora ya maisha.

Ruka Juu iliwafuata **wajasiriamali sita na biashara zao** katika maeneo yao ya kazi. Waliwekwa kwenye majaribio yaliyohusiana na uendeshaji bora wa biashara. Mshindi aliyetajwa wakati wa kipindi cha luinga kilichorushwa moja kwa moja alichaguliwa kwa kura za wananchi pamoja na majaji. Mshindi ameonyesha stadi za kweli za mjasiriamali mdogo mdogo, utayari na uwezo wa kujifunza, uelewa na kupambana na changamoto katika maisha. Washiriki wote wameonyesha stadi za kijasiriamali pamoja na za uongozi.

Femina HIP tunapenda kutoa shukrani za dhiti kwa majaji wetu pamoja na washiriki wote. Pia tunapenda kuwashukuru washirika wetu waliotuwezesha kuzalisha kipindi hiki; shukrani za pekee ziende kwa Financial Sector Deepening Trust (FSDT), AON insurance brokers, Tanzania Media Fund, National Microfinance Bank (NMB) pamoja na Sir Ronald Grierson, mchangiaji binafsi kutoka Uingereza.

Mtanzania, sasa ni wakati wa “kuruka juu na kujenga maisha yako”!!!!!!

Ruka Juu na Fema TV Show

- **Genre:** Reality entrepreneurship competition
- **Target viewership:** Youth, ages 16 - 35
- **Platform:** *Fema TV Talk Show*, a Femina HIP brand since 2003.
- **Reach:** *Fema TV Talk Show* viewers, 3.4 million
- **Name:** *Ruka Juu na Fema TV Talk Show*
- **Language:** Swahili
- **Number of contestants:** 6
- **Age of contestants:** 18 - 30
- **Prize:** 5 million Tanzanian shillings (TZS)
- **Time:** 60 minutes per episode
- **Occurrence:** Weekly
- **Number of episodes / pilot series:** 11
- **Show aired period:** 12th March – 21st May 2011
- **National Tanzanian TV broadcast stations:** ITV, TBC1 and Clouds TV